KISWAHILI (Insha na Utangulizi wa Fasihi)

KARATASI YA PILI

SEHEMU A (Alama 15)

ZOEZI LA I: INSHA

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja umusu ukimalizia kwa maneno uliyopewa.

..... hakika ilikuwa hadithi ya kusisimua.

SEHEMU B (ALAMA 35)

ZOEZI LA II: FASIHISIMULIZI (Alama 10)

1. Taja majukumu mawili ya fasihi simulizi. (alama 2)

2. Wahusika ni viumbe wa sanaa ambao hutumiwa katika kazi ya fasihi kuwasilisha maswala mbalimbali. Taja wahusika watatu katika kazi ya fasihi. (alama 3)

3. Taja tungo mbili za fasihi simulizi. (alama 2)

4. Eleza sifa mbili za fasihi simulizi. (alama 2)

5. Mbinu za lugha ni maneno au vifungu vya maneno vinavyotumika kutia fasihi urembo ili kufanya ujumbe ueleweke vyema zaidi. Andika mbinu mbili za lugha. (alama 1)

ZOEZI LA III: NOVELA (alama 10)

Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali

"Doc!" Chale aliita. "Tumefanikiwa! Tumefanikiwa! The operation was successful! Sasa umepona, mzee wangu. Maumivu tumeyazika katika kaburi la sahau," Chale alimwambia daktari Maarifa ambaye alikuwa akitiririkwa na machozi.